

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



**TANGAZO LA KUITWA KWENYE MAFUNZO YA
AWALI YA UCHUNGUZI**

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) anapenda kuwatangazia watu wote walioomba nafasi 350 za ajira ndani ya TAKUKURU kwamba mchakato wa ajira umefikia hatua ya kwenda kwenye Mafunzo ya Awali ya Uchunguzi.

Vigezo vilivyotumika katika kuwapata watu wanaotakiwa kwenda kwenye mafunzo ni pamoja na vifuatavyo;-

- Kiwango cha ufaulu wa mshiriki kwenye usaili;
- Haiba ya mshiriki; na
- Upekuzi kuhusu mwenendo wa kila mshiriki.

Mambo Muhimu ya Kuzingatia:

1. Kila mshiriki anapaswa kuhudhuria Mafunzo ya Awali ya Uchunguzi yatakayofanyika kwenye Chuo cha Polisi Moshi;
2. Kwa upande wa nafasi ya AFISA UCHUNGUZI kila mshiriki anapaswa kuripoti kwenye Chuo cha Polisi Moshi tarehe 23.4.2022 siku ya Jumamosi;
3. Kwa upande wa nafasi ya MCHUNGUZI MSAIDIZI kila mshiriki anapaswa kuripoti kwenye Chuo cha Polisi Moshi tarehe 25.6.2022 siku ya Jumamosi;
4. Maelekezo kuhusu ushiriki wa mafunzo haya yameainishwa kwenye barua ya wito.
5. Barua ya wito wa kwenda kwenye mafunzo imetumwa kwenye anwani na *email* ya kila mhusika.

Mkurugenzi Mkuu anawapongeza wote waliofanikiwa kuchaguliwa kwenda kwenye mafunzo hayo.

Imetolewa na;

Mkurugenzi Mkuu,
Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa,
Mtaa wa Jamhuri,
S.L.P 1291,
41101 DODOMA.